

Filamu ya Kiswahili: Fasihi Simulizi Iliyostawi

Gervas A. Kasiga na Neema Julius Luhwago
Chuo Kikuu cha Dodoma

Ikisiri

Makala haya yanajadili sanaa ya filamu za Kiswahili kama fasihi simulizi iliyopevuka na kuchukua mkondo wa kiteknolojia kutokana na utegemezi wake wa nyenzo za kisasa katika utambaji. Hadhi ya kisanaa ya filamu imetazamwa kwa namna inayoonesha kujitokeza kwake kupitia umbo na wajihi wa kifasihi. Filamu imeonekana kuwa jukwaa huru linaloruhusu sanaa tofauti zinazosindikiza ujenzi wa maudhui ya kifasihi kujipenyeza kusaidia kuutengeneza ujumi wa kifasihi. Kustawi kwa fasihi simulizi kupitia umbo la filamu kumechunguzwa kwa namna inavyodhihirisho taswira zilizo ndani ya bongo la mtambaji: anayezitoa na kuziweka katika picha jongefu ili mtazamaji azione runingani na kumfanya ayaone maumbo ambayo alipaswa kuyafasiri kulingana na mwendelezo wa simulizi. Ukuaji wa filamu ya Kiswahili umejadiliwa sanjari na udondokaji wa usomaji wa riwaya, tamthiliya, pamoja na ushukaji wa jumla wa kusoma nchini Tanzania. Licha ya filamu kuonekana kupiga kasi katika kueneza Kiswahili, ukuzaji wake umeonekana kutia shaka. Hivyo, imeonekana ni vyema somo la uandishi wa filamu liingizae katika mtalaa wa fasihi ya Kiswahili ili kuwajenga waandishi wa miswada ya filamu pamoja na kuongeza fursa za ajira kwa wanaKiswahili. Mwishoni, manju wa fasihi simulizi ya Kiswahili wameshauriwa kuchangamkia kukua kwa teknolojia kimawasiliano na kihifadhi wa sanaa, fasihi na utamaduni.

Maneno Muhimu: Filamu, Tamthiliya, Drama, Drama ya Runinga.

Utangulizi

Perrier (1992) anasema:

*The Study of literature casts light on the meanings in the film, and the study of the film can illuminate the full value of the literature.*¹

¹ Tazama utangulizi wa kitabu cha *From Fiction to Film* kilichohaririwa na Ronald G. Perrier na kupigwa chapa na *Archie publication* mwaka 1992.

Fasihi hutoa mwangaza katika kuleta maana ya filamu, vivyo hivyo, filamu huzidi kupamba thamani ya jumla ya fasihi. (Tafsiri yetu)

Awali, filamu haikuchukuliwa kama sehemu ya sanaa inayoweza kutoa maumbo yenye kuleta maana, mafunzo, na uburudishaji kwa wana-jamii. Jambo hilo lilitokana na filamu kuwa imetazamwa zaidi kwa jicho la kisayansi na kiteknolojia na, hivyo, kuondolewa hadhi yake ya *ki-insia* hasa hasa katika utumiaji wake wa lugha katika kufanikisha lengo kuu la mawasiliano kwa walengwa wake ambao ni hadhira mahususi.

Kwa lugha nyepesi tunaweza kusema kuwa filamu ilitazamwa kama chombo chenye kurudufu maisha kama yanavyoonekana bila ya unogeshwaji wowote ambao ndio unaorejelea dhana ya sanaa ya lugha inayopatikana ndani ya filamu. Vilevile, kwa kipindi kirefu filamu imekuwa ikitazamwa kwa dhana ya utayarishaji kupitia vigezo vya utumiaji wa vifaa vinavyochukua picha jongefu, uhariri wake, mbinu za uchukuaji wa picha jongefu na mkabala wake ulio wa karibu kibiashara, na pia kiuburubishaji. Kwa mintarafu hiyo, utayarishaji wa filamu ulikuwa ukiangaliwa zaidi kwa muktadha wa uingizwaji wa kipato kupitia hadhira yake inayopaswa kununua mikanda yenye filamu ili waweze kupata burudani.

Iisahaulika kuwa, filamu nayo hudondoa yale yanayopatikana katika fasihi. Fasihi na filamu ni tiba mbili za asili moja zenye kuelekea katika hitimisho moja lililopita katika njia mbili tofauti. Hii ni sawa na kusema kwamba fasihi ni sawa na kidonge cha tiba kinachomezwa kisha kuchukua hatua ya ngazi kwa ngazi katika kuleta uponyaji lakini filamu ni sindano inayotoa dawa iingiayo moja kwa moja katika mishipa ya damu na kutoa uponyaji wa papo hapo. Utamazaji wa filamu humuacha mtazamaji akilipuliwa na sauti asizikiazoo, picha zenye matukio mbalimbali ayaonayo na hivyo kusababisha hisia kuujaa mwili wake kadiri hadithi inayotambwa inavyoyabadilisha matukio ayaonayo. Hivyo basi, mtakaso wa kihisia, tulizo, maliwazo, burudiko pamoja na uepaji wa matatizo kupitia burudiko la kisanii vyote hujidhihiri sawa sawa na vile linavyojiyakini kupitia fasihi.

Maandiko ya lugha, fasihi ya Kiswahili na sanaa za maonesho yaliyopitiwa hayauoneshi udugu uliopo baina ya sanaa hizi mbili za fasihi na filamu. Sanaa hii ya filamu haikupewa mtazamo wake stahili kwa upande wa hadithi zinazotambwa ndani yake na kuhifadhiwa kwa kutumia vifaa vya usasa vya kiteknolojia. Mengi ya maandiko na tafiti za lugha mara nyingi zimekuwa zimekiichanganua filamu kupitia maudhui na ujumbe unaotolewa na filamu bila ya kuangalia kuwa: kiujenzi na kiukuaji tumbo la fasihi ndilo limezaa sanaa ya filamu.

Maandishi ya sanaa za maonesho nayo yameipeleka filamu katika eneo la uoneshaji na utendaji wa vitendo pekee. Kwa upande mwingine, yamesahau kuwa sanaa hii ya filamu inabebwa na hisia kubwa yenye mguso wa karibu kabisa wa

hisia za binadamu wa kawaida kutoka utamaduni wa jamii iliyolengwa na hadithi ione kanayo mbele za runinga. Ukaribu huo wa kihisia na mtazamo hauwezi kudhihirika vyema bila ya uwepo wa filamu katika maisha haya yaliyonakshiwa na usasa. Maandiko hayo yamelijaza vyema eneo la sanaa kupitia namna vijenzi vya kiteknolojia vinavyoweza kumsaidia muongozaji wa filamu kuisimulia vyema hadithi yake huku kiini cha kuwepo kwa filamu, yaani hadithi ya kutambwa, ikiachwa ikieng' aeng' a. Eneo hili la hadithi lililoachwa pweke katika majadiliano mengi ya kitaaluma ndilo chanzo cha filamu na ukuaji wa fasihi uliovuka mipaka ya kijadi na kuelekea katika teknolojia. Kwa mantiki haya, filamu haiwezi kuwa bila ya jambo la kusema ama suala la kujadililiwa. Suala hilo la kusema ndilo hadithi inayobunilizwa mbele ya runinga kwa kupitia nyenzo za kiteknolojia. Hivyo, kwetu hiyo ndiyo filamu tunayoiangazia katika makala haya.

Kwa hivyo, makala haya, yanaifafanua dhana ya filamu kama hadithi yeyote inayotambwa kupitia picha jongefu. Sifa hiyo ya kipekee ndiyo huifanya filamu ijitwalie hadhi ya kuwa sanaa ya fasihi simulizi iliyopevuka si kwa utumiaji wa lugha pekee, bali hata kwa uwezo wake wa kuwa jukwaa huru linaloruhusu sanaa nyingine kujipambanua kupitia kwayo.

Usanaa wa Filamu

Kabla ya kwenda mbele zaidi, itakuwa ni vizuri tukiubainisha usanaa wa filamu. Mosi, kwa kuibainisha dhana nzima ya sanaa na kisha kuangalia namna filamu inavyoweza kujiinua kwa kupitia maumbo mbalimbali ya kisanii. Kwa ufupi, sanaa chombo chenye uwezo wa kuakisi maisha: yaani kioo, dhahania, au sehemu ioneshayo jinsi tunavyoishi, tunavyofikiria na tunavyohisi. Kwa kupitia sanaa, mambo tunayovutika nayo, na vitu tunavyovithamini sana huwekwa dhahiri shayiri. Si hivyo tu, sanaa huwa na ujasiri wa kuyajadili masuala ya kijamii, kiutamaduni na kisiasa yanayoogofya watu, yasiyofikiriwa kujaribiwa kuzungumzwa katika njia nyingine zisizo na udugu wa kisanana.

Mawazo na hisia za mwanadamu haziwezi kuoneshwa kirahisi kwa njia tofauti zaidi ya njia zilizofumwa kisanana. Sanaa huonesha mahangaiko ya mwanadamu katika kuyakabili maisha yake ya kila siku kwa sura ya kipekee. Uwasilishaji wa mawazo yenye kuakisi ukweli hujengwa katika namna yenye kuongezwa chuku na msanii ili aweze kuupalilia vyema ukweli anaoutarajia kuusema, kuuonesha au kuuweka mbele ya hadhira yake kupitia sanaa yake aliyoibuni. Ubunilizi huo wa kinjozi ndiyo husukuma, huchochea, husababisha ujenzi, na uhai wa sanaa.

Uzuri wa sura ya kitu unaweza kuoneshwa vyema kwenye mchoro wa rangi kuliko ambavyo ungeelezwa kwa maneno; haiba yaweza kuelezwa vyema kwenye nathari au tamthiliya kiasi cha kuweza kuwasilisha hisia ya ndani ya nafsi ya mwanadamu; furaha au maumivu makali ya moyo yanaweza kuwasilishwa

kwa haraka kupitia muziki, ushairi, drama ya jukwaani ama runingani, au filamu kuliko njia nyingine za kisanaa. Yote hii ni kusema kuwa bila ya njia hizi za mawasiliano, maisha ya wanajamii yangekuwa hayana msisimko kama vile ambavyo jamii ingethubutu kuishi bila ya lugha irejeayo mawasiliano yao ya kila siku. Kwa kuwa tu hai, tunaishi, basi maisha yetu na utu wetu sisi wanadamu hauna ujanja wa kukwepa njia hizi za kisanaa za kuwasiliana: aidha ziwe za kijadi au za kisasa. Yote hiyo ikiwa ni kwa minajili ya kuyafanya maisha yetu yasongee bila tabu.

Basi kwa unyumbulishaji wa kuleta mantiki ya mapema, tunaweza kusema kuwa, sanaa inagawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni; sanaa za fasihi, sanaa za fani, na sanaa za maonesho. Sanaa za fasihi zinahusisha miviga, ngano, nathari, hadithi fupi, tamthiliya na ushairi. Sanaa za fani zina jumuisisha michoro ya rangi, ufinyanzi, sanaa za uchoraji majengo, na sanaa ya upigaji picha mnato na uchukuaji picha jongefu. Sanaa za maonesho hujumuisha drama, ngoma, *opera*, na muziki. Sanaa ya filamu ni sanaa ngeni lakini inayokua kwa kasi. Sanaa hii hujibua katika makundi yote matatu yaani sanaa za kifasihi, sanaa za fani na sanaa za maonesho.

Hivyo, kama tulivyokwisha kutanabaisha awali, kumea kwa filamu kutoka kwenye mizizi ya fasihi ni kukubwa kuliko kwenye sanaa nyingine nilizozitaja. Sanaa zote zilizobakia hubakia zikiwa zinaujenga uzuri unaooneshwa runingani kupitia hadithi inayosimuliwa (Kasiga, 2013). Uzuri huo huonekana kupitia picha jongefu zinazosaidiwa na muziki au mapigo ya kimuziki katika “utambaji wa hadithi”. Wakati mwingine kunaweza kukawa na uwepo wa picha jongefu zenye kupamba mandhari ya hadithi kwa kuonesha majengo yenye mvuto wa kisanaa. Pia uwepo wa sebule ama vyumba vyenye mapambo ya kuvutia, maleba pamoja na mavazi ya waigizaji yaliyobuniwa kulandana na husika pamoja na hisia ya vipande vya hadithi inayotambwa. Vyote hivyo haviachi kujumuisha uzuri kutoka maumbo ya sanaa nyingine tofauti zinazofurahia uwepo wa jukwaa zuri la filamu.

Katika fasihi, filamu hujitokeza kupitia kupitia umbo lake linalobebwa na hadithi pamoja na mbinu za usimuliaji/utambaji. Utambaji wa hadithi ya filamu hutokana mfululizo wa picha jongefu zilizobeba hadithi zinazotambwa runingani. Mfululizo huo wa picha jongefu huwa sawa na mfululizo wa maneno simulizi yanayosemwa na kutambwa na manju au yanayokuwa kwenye karatasi ambayo msomaji huyasoma. Aidha, kujitokeza kwa filamu kwenye fasihi huwa katika utambaji wa hadithi kutoka maneno ya mtambaji/manju kwenda kwa hadhira. Matumizi ya lugha kupitia daiolojia inayosemwa na wasanii wa filamu huonesha jinsi filamu inavyozaliwa kutoka kwenye tumbo la fasihi. Hiyo ni kusema kuwa wajihi wa filamu umerithiwa kutoka kwa fasihi (Kasiga, 2013).

Jambo muhimu linaloweza kuzipa tofauti kiasi ni uwepo wa hadhira. Kwa mfano, nathari imekaa kibepari kwa kuwalenga wale wajuao kusoma tu, na

wakati huo huo husomwa na msomaji mmoja pekee anayejichagulia mahala pa kukaa kuisoma riwaya yake na kuliwazika, au hata kuchomeka na ayasomayo. Filamu yenyewe ina mrengo wa kijamaa zaidi ambapo mtu pekee anaweza kununua mkanda wake wenye filamu na kuweza kuuangalia pekee, na familia yake, kuzunguka na gari la kuoneshea filamu na kuionesha kwa jamii pana au hata kwenda katika jumba la kuoneshea filamu kuonywa, kuburudishwa na kujamalika kwa masuala mbalimbali yaliyofungwa katika hadithi inayotambwa.

Kama ilivyo kwa fasihi, filamu huwa na hadithi, wahusika, mfululizo wa matukio yaliyobeba hisia, utumiaji wa taswira mbalimbali na maneno, pamoja na dayolojia zenye maneno kutoka lugha yeyote izungumzwayo na wanadamu. Kutokana na kuwa sehemu ya sanaa za kifasihi, filamu huambatana na mbinu simulizi za upangaji wa majukwaa ya kutambua hadithi, mijongeo ya wahusika, nyimbo na matumizi ya ishara. Haitoshei hapo tu, ukizidi kuihusisha na nathari, filamu huwa na muundo, uhusika na wahusika, dhamira na mtazamo fulani unaolegwa na msanii muundaji wa kazi hiyo.

Kupitia kujizatiti kwake kwenye fasihi kwa kupitia ushairi, filamu inajijenga kupitia matumizi ya sitiari, ishara na mbinu nyinginezo za kifasihi. Filamu kama ilivyo ushairi yaweza kuelezea furaha ya kupita kiasi na maumivu makali ya mtu. Kupitia muziki na dansi filamu huwa na mahadhi ya kimuziki, marudio marudio na ujalizaji/utumbuizo. Vilevile mpangilio wa nathari nao umestawishwa kwenye filamu. Katika nathari kuna maneno, sentensi, paragrafu, sura, na kupata hadithi ya nathari nzima. Katika utambaji wa filamu kuna fremu ya picha jongefu na kipande kidogo cha hadithi ya mchezo ambavyo vikiunganishwa huleta dhana nzima ya mfululizo wa hadithi ya filamu. Hiyo ni sawa na kusema kuwa: sanaa ya maneno inayojenga dhana ya fasihi na sanaa ya picha jongefu iliyopo kwenye filamu ni dhana zinazofanana. Dhana zote mbili za usomaji na utazamaji huanzia jichoni ili kuleta kujenga mantiki ya sanaa inayotambwa mdomoni na kusikilizwa, inayosomwa kitabuni na kutafakariwa ama inayotazamwa runingani na kusikilizwa. Yote hiyo hujielekeza katika kusudi la kupata maana mahususi iliyofungwa na kufichwa ndani kazi ya kifasihi. Katika kutafuta eneo linalotupatia mahusiano kati ya fasihi na filamu. Kileo (2011) anasema:

Filamu, kama kipengele cha fasihi, ni utanzu wa drama ambao una nafasi kubwa katika kufikisha ujumbe kwa jamii, kwa sababu hadhira hupata ujumbe kwa kusikiliza maneno na kuangalia matendo yanayoigizwa na wahusika...²

² Tazama “Nafasi ya Maudhui ya Filamu za Kiswahili katika kuakisi masuala ya Kijamii: Uhakiki wa Filamu za Taswira na Vita vya Ushindi”, Tasnifu ya Shahada ya Umahiri

Ukichungua mtazamo huu utaona umeihusisha filamu kama kipengele cha drama ambacho kipo kwenye sanaa za maonesho pekee. Bado uhusiano baina ya filamu na fasihi haukuweza kuoneshwa kwa bayana. Ukitazama kwa umakini utagundua kuwa drama si tawi lililoko ndani ya fasihi bali ni kipengele kinachopatikana katika tukio lolote na mchezo wowote wenye tendo la kuigizwa, filamu ikiwemo. Kipengele hicho uhusisha matendo ya wahusika wanayofanya stejini au runingani pamoja na hisia wanazozibeba. Wakati mwingine huonesha hisia na matendo ya wahusika wa kingano yanayotambwa na manju kwa kushirikiana na hadhira tendaji wakati wa utambaji. Katika kuendelea kutafuta ukweli katika uunganishaji wa mahusiano ya dhana hizi mbili yaani tamthiliya na filamu akirejelea filamu za Kiswahili za Marehemu Steven Kanumba. Suwed (2013) anasema:

Tamthilia ni utanzu wa fasihi ambao huwa na majibizano ya wahusika pamoja na vitendo. Kuna tamthilia andishi na simulizi; na hivyo tuseme tamthilia huweza kuwa kipengele cha fasihi andishi na simulizi (Mulokozi, 1996). Katika siku za hivi karibuni tamthilia hizi zimerekodiwa katika filamu na kuuzwa. Moja ya filamu maarufu nchini Tanzania na katika nchi nyingine za Afrika Mashariki ni filamu za Steven Kanumba.³

Kwa maelezo hayo, cha kwanza, yanatupatia mwangaza katika kutusaidia kuuona ukomavu wa filamu kutoka sura na wajihi wa fasihi simulizi ila kwa upande mwingine bado ametuachia mkanganyiko wa kimuktadha pindi anapoihusisha filamu na drama. Kupitia nukuu yake bado utata umebaki ukionekana katika tafsiri na utendaji baina ya hii mikondo miwili ya sanaa ya lugha. Hapa tunaona kwamba filamu imetazamwa kama zao la tamthiliya lakini ukitazama kiutendaji hizi ni sanaa mbili zenye kutaka kufanana kwa msingi ya kuwa zote ndani yake zina tendo la kuigizwa ingawa utendaji wake ni wa tofauti kabisa. Hapa kuna dhana ya tamthiliya iliyoandikwa kitabuni ambayo inapotendwa utendaji wake huipa umbo la kisanaa na kuifanya iwe drama. Katika kuikazia hoja hii, Hussein (1983, 2008) anasema:

katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (2011) iliyoandikwa na Scholastica Egbert Kileo, Ukurasa wa 4.

³ Tazama “Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha Katika Filamu za Steven Kanumba”, Tasnifu ya Shahada ya Digrii ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2013) iliyoandikwa na Ahmad Abdala Suwed, ukurasa wa 12.

Mwandishi wa tamthiliya baada ya kuipata fikira ya kishairi⁴ na baada ya kuwa nayo kwa muda anaweza kufanya moja katika mawili: anaweza kutafuta kalamu na karatasi (haidhuru hata mashine ya kuchapia) au anaweza kwenda jukwaani ili kuipa fikira hiyo umbo la kisanaa. Akitenda la kwanza basi huwa anaipeleka tamthiliya kwenye fasihi. Akitenda la pili basi basi huwa anaipeleka tamthiliya kwenye mazingira yake ya ulimwengu wa jukwaa...⁵

Waidha, katika kuendelea kuifafanua dhana hii ya drama, Brockett (2003) anaainisha drama kwa kusema kuwa ni uakisiaji wa mtu akiwa kitendoni, lakini kitendo hicho hakimaanishi mijongeo ya kimwili pekee pia uhusisha vichochezi vingine haswa vya ki-bongo na kisaikolojia vyenye matendo yaliyodhahiri. Vilevile, hujumuisha hisia, mawazo na matukio ambayo humpa taswira mwanadamu kuwa yu kiumbe wa namna ipi, kwa kupitia yale anayoyatenda, na kwanini anayatenda hivyo.

Tukiirejelea dhana ya Drama ya Runinga ili kuitolea ufafanuzi, Kisner (2004) anaieleza kuwa ni midia yenye kuhusisha jicho. Anasema drama hizi huwa na hadithi zinazosimuliwa kupitia “vilele vya mlolongo wa matendo yenye kuonekana”⁶. Na hiyo ni kwa sababu jicho huweza kuona matendo, kwa hiyo, kama ilivyo kwa filamu, Drama ya Runingani nayo ni lazima itumie taswira halisi. Licha ya hayo, bado filamu haiwezi kuwa sehemu ya drama ya runinga kwa sababu drama ya runinga huwa na visa vingi vya hadithi vinavyotambwa kupitia vilele vya hadithi hiyo, wakati mwingine, kwa kuwa na uendelevu wa kihadithi usiokwisha kwa kuakisia kwamba maisha (kwa dhana pana) hayana mwisho. Kwa upande wa pili, filamu huwa na hadithi iliyobeba kisa kimoja kinachoanza, kukua, kufikia kilele na kupata hitimisho. Kwa hiyo, hapo ni sawa na kusema kuwa kilele cha kisa (drama) ni sehemu moja tu ya mfululizo wa filamu sawasawa na kusema hivi: drama ni sehemu ya filamu na si filamu kuwa sehemu ya drama. Kwa maneno mepesi tunaweza kusema hivi: filamu hubeba hadithi yenye kisa kimoja kinachoanza, kupevuka na kukua (ambapo drama

⁴ Katika makala haya “fikira ya kishairi” anayoizungumzia Ebrahimu Hussein imetazamwa kama “njozi ya kibunilizi”.

⁵ Tazama “Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthiliya Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle, Makala kutoka Jarida la Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III lililochapishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Mwaka 1983 na 2003. Makala hii imeandikwa na Ebrahim Hussein, ukurasa wa 197.

⁶ Msisitizo ni wetu.

hujidhihiri) na kisha hadithi hiyo kupata hitimisho lake kwa mantiki ya kuupoza mgogoro ulioibuka.

Katika kuendelea kutafuta mahusiano ya kinasaba kati ya filamu na fasihi huku tukijaribu kuuepusha mkanganyiko wa kiufafanuzi uliopo sasa kuhusu dhana tatu za Tamthiliya, Drama ya Runinga na Filamu, Nyoni (2001) anasema:

Tofauti kubwa na ya msingi iliyopo kati ya drama na filamu ni kuwa drama inaangalia zaidi migogoro wakati filamu hushughulikia zaidi maendeleo katika kufikia au kutatua mgogoro fulani (*“drama is the art of crisis, as movie is the art of development”*). *Dramatists must begin when the situation is coming to a boil, not when the fire is first lighted*. Uchaguzi wa mambo gani yaonyeshwe ni muhimu sana katika utengenezaji wa drama. Tukumbuke kwamba katika drama tunaonyesha yale tu ambayo yanachangia katika kukamilisha lengo. Kinachotokea katika drama ni sehemu tu ya hadithi nzima, yaliyobaki hufanyika nje ya drama, katikaki ya maonyesho, au kabla ya drama yenyewe kuanza. Hata hivyo, yanayofanyika nje ya drama lazima yadokezwe katika matendo au maneno yanayosemwa.⁷

Mlaga (2017) anaitazama filamu kama tawi jipya la fasihi kwa kuiona kuwa ni fasihi Elektronik. Msingi wake mkubwa wa hoja bado umelalia katika namna teknolojia inavyoweza kusaidia “kutamba” (kusimulia) hadithi hususani katika kipindi hiki cha maendeleo ya kisayansi. Anasema kuwa wataalamu wengi wameshafanyia uanishaji wa fasihi ya Kiswahili. Mathalani Mulokozi (1996) na Wamitila (2006) ambao wamefanya uainishaji wa fasihi ya Kiswahili kwa kubainisha mgawanyo tanzu kuu mbili: fasihi simulizi na fasihi andishi. Anasema wataalamu wote hawa wanakiri kuwa fasihi ni moja tu bila kujali kuwa ni andishi au simulizi. Alichokiona ni kuwa wataalamu hawa hawakusogea mbele kuangalia tanzu mpya zilizoinuka katika kipindi cha ukuaji wa kisayansi ambazo zina sifa zote za kifasihi. Tanzu hizo kama filamu, maigizo ya runinga, vibonzo jongefu, futuhi au komedi za runingani, nyimbo za bongofleva, na michezo ya redioni. Mlaga (khj) anatusaidia sana kuyaonesha mahusiano baina ya filamu na fasihi na pia katika kuelekea kulijenga lengo letu la pili la makala haya la kuibua mjadala wa kwanini filamu haifundishi katika masomo ya fasihi ya Kiswahili ili kuongeza fursa ya ajira kwa wanafunzi wa masomo hayo. Vilevile, anatusaidia kuona

⁷ Tazama Utaalamu katika Utengenezaji wa Drama za Runinga, Makala yaliyotayarishwa na Frowin Paul Nyoni kisha kuwasilishwa katika Kongamano la Maendeleo ya Sanaa za Maonyesho Tanzania lililofanyika Dodoma, Tanzania 19-21-2001.

teknolojia inavyoitana fasihi kutoka kwenye dhana ya awali ya masimulizi ya njia ya mdomo hadi katika usaidizi wa utambaji kupitia vifaa vya kiteknolojia.

Mahenge (2016) anatoa tafsiri ya filamu kwa kuanza kwa kujenga hoja yake kutoka kwa Kileo (2011) na Kasiga (2013). Anaiona filamu kuwa ni utanzu fasihi unaotumia picha jongefu na mbinu za kifilamu kuwasilisha “hadithi” inayosimuliwa na watu wengi. Watu wengi hao anaeleza kuwa ni mwandishi wa mswada, mpigapicha, msimulizi, mhariri na mwigizaji ambao wote husaidiana kusimulia hadithi. Mahenge anasema japokuwa Kasiga (2013) amejitahidi kutaja mambo muhimu yanayohusiana na filamu, lakini kuna vitu vya msingi ameviacha. Mahenge (khj) anaongezea sifa ya ujumishi (*maltimodo*) ambayo inaipambanua filamu na aina zingine za sanaa. Kwetu sisi sifa hii ya ujumishi ndiyo tunaiona kuwa ni sifa inayoifanya filamu kuwa jukwaa huru linaloipa filamu nafasi ya kuruhusu sanaa nyingine kujipambanua kupitia filamu katika kuujenga ujumi wa kifasihi unaooneshwa na filamu. Licha ya sifa hii kuletwa na teknolojia haiondoi dhana ya masimulizi ya hadithi ambayo ndiyo kiini cha filamu.

Mtazamo wa Mahenge (khj) haukubaliani kuwa filamu ni sehemu ya drama ingawa kwa kiasi fulani anakubaliana na mtazamo wa kuuona ufasihi katika filamu kwa kusema kuwa mwingiliano wa filamu na fasihi unatokana na kuwepo hadithi inayotambwa, wahusika, matumizi ya hisia na taswira mbalimbali, pamoja na daiolojia zenye maneno kutoka katika lugha yeyote izungumzwayo na wanadamu kwa kumnukuu Kasiga (2013). Anaiona filamu ni fasihi jongefu inayosimuliwa na watu wengi kwa kutumia lugha za aina mbili; yaani lugha ya kifilamu na lugha ya kawaida inayozungumzwa na wanadamu. Ufasihi jongefu wa filamu anaouona Mahenge katika makala haya tunauona kama ni ukuaji wa fasihi simulizi kupitia usaidizi nyenzo za kiteknolojia katika usimuliaji (utambaji) wa hadithi.

Kupitia uchambuzi wa mapitio ya marejeleo kuhusu fasihi na filamu yaliyotajwa awali, tunaiona filamu kama fasihi simulizi iliyostawi kutokana na utambaji wake uliovuka mipaka ya kijadi na kuelekea kwenye vifaa vya kiteknolojia vinavyomsaidia manju kutamba hadithi na kuifikia hadhira kwa mawanda mapana. Vitu vinavyoifanya filamu kuwa fasihi simulizi ni uwepo wa hadithi inayotambwa, upangaji wa matukio, msimuliaji/mtambaji (muongozaji wa filamu), matumizi ya nyimbo na fani mbalimbali za kijadi, upangaji wa vionwa, maleba, na matumizi ya lugha kupitia daiolojia zinazozungumzwa na waigizaji. Kwa tafsiri hiyo utaona kuwa filamu si sehemu ya drama ila drama ni sehemu mojawapo inayounda hadithi ya filamu hasa pale mivutano kati ya mhusika mkuu na mhusika mpinzani, adui au mchokozi na kani zao zinazokinzana zinapokamata hatamu katikati ya filamu na kisha kuisukuma hadithi kwenye kilele cha mgogoro huo ili kuelekea kutafuta hitimisho.

Kwa hiyo tukumbuke kuwa utambaji wa filamu huongozwa kupitia usaidizi wa vifaa vya kiteknolojia kama vile, kamera ya picha jongefu, vifaa vya mwanga, vifaa vya sauti, nyenzo za uhariri na kadhalika. Kutokana na usaidizi wa vifaa hivyo manju hubadilika kutoka usimuliaji wa hadithi kwa njia ya mdomo na kumfanya awe muongozaji wa filamu. Hivyo basi, makala haya yanaendelea kujizatiti kuitazama sanaa ya filamu kama tanzu ya fasihi simulizi ambayo usimuliaji wake una mbeleko ya nyenzo za kiteknolojia. Hatuingii wahaka kusema kuwa: kwa dhana ya hadithi au simulio ambayo ndiyo filamu ilikuwepo kabla ya maendeleo ya kiteknolojia na imekuwa ikibadilika kadiri jamii inavyokua kisayansi na inavyokabiliana na changamoto kemkem za kimaisha. Katika kuzidi kuthibitisha hili tunaweza kulihusisha na suala la ndoto za mwanadamu na uwepo wa filamu kabla ya kuwepo kwa teknolojia yake. Kila mwanadamu ameshawahi kuota na anaendelea kuota siku hadi siku kadiri mawazo yanavyoigonga akili yake iwe kwa furaha, maumivu, chuki na kadhalika. Kila anayeota ndoto huyaona maumbo yenye picha halisi yakitembea kichwani kwake, yakitoa simulizi ama kutamba jambo fulani. Jambo hilo hupitia milolongo yote ya hadithi tuionayo leo hii katika filamu. Kila ndoto lazima iwe na mwanzo wa hadithi kati na hitimisho la simulizi alipatalo kupitia utambaji wa bongo lake. Hivyo ukitazama kwa makini utaona kuwa uwepo wa filamu ni lulu kwa mtambaji yeyote kwani ni njia maridhawa yenye kumsaidia kutoa maumbo na maana stahiki aliyonayo ndani bongo lake lililosukumwa na ubunilizi wa kinjozi.

Fauka ya hayo, ili hadithi iliyofungwa ndani ya filamu iweze kuhadithiwa vyema, filamu bado huwa haina budi kuzidisha kutumia mbinu nyingine za kisanaa zilizombali na lugha kwa minajili ya kuleta ukamilifu wa filamu. Mbinu hizo huhusishwa utumiaji wa maleba na mavazi maalumu ili kuyajenga mandhari na kuzikamilisha vyema husika kwa waigizaji wanaobeba husika hizo. Zaidi ya hayo, uchukuaji picha jongefu nao huwa wa kibunifu unaoendana na sababu mahususi ambayo muongozaji wa filamu anaihitaji katika kujenga maana aliyokusudia. Ubunifu hauishii kwenye uchuaji wa picha jongefu tu bali huzidi kutumika hadi kwenye uhariri wa picha jongefu ili kuleta ukamilifu wa filamu.

Filamu kiziwanda cha Fasihi Andishi, kijukuu cha Fasihi Simulizi, kilembwe cha Utamaduni wa Ki-Afrika

Katika kuitanua na kuiongezea nyama tafsiri ya filamu zaidi ya tulivyoifafanua hapo mwanzoni, ingekuwa vyema kunawirisha maelezo ya filamu kwa kusema kwamba ni hadithi yeyote inayotambwa kutoka kwa waongozaji wake kupitia picha jongefu zilizorekodiwa kutoka kwenye mazingira fulani. Hadithi hizo huwahusisha waigizaji kutoka kwenye jamii inayoendana na mazingira yao, desturi zao, pamoja na utamaduni uendao sambamba na mawasilisho ya maudhui yaliyosanwa vyema kwenye filamu hizo. Picha jongefu zinazochukuliwa ili kutayarishia filamu hurekodiwa kutoka kwenye mandhari fulani kupitia kifaa cha

kurekodi kiitwacho kamera ama kwa kutumia teknolojia ya katuni au kwa kutumia umahususi wa picha wenye kuleta athari baada ya uhariri wa picha hizo.

Kama ilivyo kwa sanaa yeyote ile ya kifasihi, filamu nayo huwa ni zao la utamaduni linalobeba ubunifu kutoka kwenye silika ya jamii fulani iliyolengwa. Utamaduni au mawazo hayo hulenga kuleta athari iliyokusudiwa kuonekana kwa jamii hiyo kutoka kwa mtayarishaji wa filamu. Sanaa hii ni muhimu sana. Endapo ikijengwa vyema huwa ni sanaa madhubuti yenye uwezo wa kuiburudisha jamii kwa mawanda mapana na papo hapo ikiwa ni njia imara ya kutolea elimu. Vilevile, filamu ni sanaa yenye uwezo wa kufunda na kutoa kasumba fulani iliyolengwa kwa jamii inayopelekewa filamu hiyo. Ujongefu wake wa picha huipa nguvu kubwa katika kuleta athari kubwa ya kimawasiliano kwa mtazamaji wake. Kwa namna nyingine, filamu zimeweza kuwa maarufu kwa jamii tofauti na ile iliyolengwa awali pale tu zinapowekwa lugha mbalimbali (*Dubbing*) ama pia kuwekewa tafsiri (*Subtitles*) za lugha tofauti katika simulizi na daiolojia zilizomo kwenye filamu.

Hadi hivi sasa, sanaa hii ya filamu imebaki kuwa njia ya kimasiliano isiyopitwa na muda toka nyenzo za kutayarishia filamu zilipoasisiwa mwaka 1894 na ndugu Louise Lumière na August Lumière.⁸ Utayarishaji wa filamu umekuwa ni sehemu ambayo watayarishaji hupata nafasi ya kuyasema mawazo na hisia zao. Filamu imeweza kuchukua nafasi ya sanaa ya jukwaani iliyokuwa kwenye kipindi cha Elizabeti (*Elizabethan time*) na vilevile, imeweza kumeza nafasi ya riwaya kwenye karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20⁹. Kupitia filamu, kila umbo na maana yake hupatiwa ufafanuzi kupitia mawazo yaliyojaa usasa. Sanaa hii ya filamu imeweza kuruka vikwazo vyote vya kitaifa, kitamaduni, kiitikadi na kidini ambapo hapo kabla hakuna sanaa iliyoweza kuvuka vikwazo hivyo kwa urahisi. Hii imetokana na kuwa filamu inaweza kutazamwa mitandaoni, hususani kwenye mitandao inayohusu filamu pamoja na mitandao ya kijamii kama vile *You-Tube*, *Facebook*, *Instagram*, na *Twitter*.

Ni vyema pia kutambua kwamba bara letu la Afrika lina utamaduni wa fasihi simulizi uliojidhatiti kwa kipindi kirefu. Utamaduni huu wa kifasihi umekuwa na athari kwa maisha ya usasa ya Wa-Afrika. Filamu ikiwa ni mojawapo ya njia ya

⁸ Tazama kitabu cha *Film Makers on Film Making* kilichohaririwa na Harry M. Geduld na kupigwa chapa na *Pelican Book*, sura ya kwanza, ukurasa wa 33 – 39.

⁹ Tazama kitabu cha *Directing Film: Techniques and Aesthetics* kilichoandikwa na Michael Rabiger na kupigwa chapa na *Focal Press*, sura ya 1, ukurasa wa 3.

mawasiliano katika maisha katu haiwezi kujitenga na muungano wenye mizizi imara ya kitamaduni uliopo kati yake na fasihi simulizi (Kasiga, 2013). Tokea mwanzoni mwa maisha, mwanadamu amekuwa akijiwa na kiu ya kuyafahamu vyema mazingira yake. Katika mahangaiko hayo amejikuta akiumba hadithi zinazomuelezea ili aweze kuitii kiu yake ya kujifahamu. Hadithi zimekuwa si kwa ajili ya ufahamu tu bali zinamsaidia mwanadamu kupata tulizo na burudani (Diang'a 2013; Hussein 2005). Kwa mantiki hayo filamu nayo kama hadithi isimuliwayo kupitia picha jongefu nayo imekuwa ikijionesha kupitia njia hii.

Filamu za Ki-Afrika zimejengwa kwa msingi wa ubunilizi wa kisimulizi wenye haiba ya uneni. Misingi hiyo imezifanya ziende sambamba na midundo ya ngoma za kiasili, nyimbo pamoja na uchezaji. Hadithi zinazotambwa pia zimekuwa zikiibuka kutoka kwenye fasihi simulizi. Baadhi ya filamu zenye amali hizi ni : *Wendi Kuun* (1983) iliyoongozwa na Gaston Kaboré, *Tilai* (1990) iliyoongozwa na Idrissa Ouedraogo, *Xala* (1975) iliyoongozwa na Ousmane Sembene. Nyingine ni: *Touki Bouki* (1973) iliyoongozwa na Djibril Diop Mambéty, *Yeleen* (1987) iliyoongozwa na Souleymane Cisse. Vilevile, kuna *Maangamizi* (1998) iliyoongozwa na Martin Mhando, *Arusi ya Mariam* (1985) iliyoongozwa na Ron Mulvihill/Martin Mhando, *La Vie est Belle* (1987) iliyoongozwa na Mweze Ngangura.

Kwa mantiki hiyo kupitia mrengo wa Ki-Afrika utaona kuwa filamu ni tawi la fasihi simulizi ambayo pia imezaa fasihi andishi. Maendeleo ya teknolojia ndiyo yanayoihamisha fasihi simulizi Ki-Afrika kutoka katika njia ya utambaji wa vitendo vya uigizaji kupitia maneno yatokayo kwa njia ya uzungumzaji wa mdomo kwenda katika maandishi na kuingia katika kamera na runinga. Watayarishaji wengi wa filamu za Ki-Afrika wanajishikiza kwenye fasihi simulizi kwa kiwango kikubwa. Masimulizi ya kifasihi huibua taswira zinazobeba picha zionekanazo kwenye mawazo ya hadhira kupitia usikilizaji wake ama usomaji wake. Filamu imekuwa ni muendelezo wa picha hizo ambazo hupata nafasi ya kuonekana moja kwa moja machoni mwa mtazamaji na kuleta athari iliyokusudiwa papo hapo bila ya kukawia.

Kwa hivyo, sanaa nzuri ya kifasihi inayotambwa au inayosomwa ni ile yenye kuyafinyanga maumbo na kisha kuibua picha zenye kuweza kuonekana mawazoni mwa msikilizaji ama msomaji ili aweze kuyatazama matukio yanayotambwa na kupata dhana zinazozungumzwa. Picha hizo huwa zinajengwa kutokana na maneno au maandishi yanayotoka kwa manju au mwandishi wa hadithi. Hivyo, filamu imekuwa mwendelezo wa fasihi simulizi kwa kuwa fasihi ya kuona vitendo vilivyondani ya simulizi vikitendwa na waigizaji runingani. Filamu ya Kiswahili nayo imeitana dhana ya fasihi simulizi kwa mawanda mapana. Kutokana na dhana ya kuandikika, miswada ya filamu nayo inahusika moja kwa moja kwenye fasihi ikiwa inashabihiana na uandishi wa tamthiliya kabla ya kuwa mchezo wa kuigiza/drama pindi unapoichukua nafasi yake stahiki

ya utendwaji wake kupitia waigizaji mbalimbali wanaoanena maneno yaliyo katika mfumo wa majibizano na kuyatenda matendo juu ya jukwaa, mbele ya hadhira.

Kwanini filamu haifundishwi mashuleni, vyuoni katika kunyayua weledi wake, kukuza lugha ya Kiswahili, na utamaduni wa Mtanzania?

Kuna maswali ambayo tunaweza kujiuliza kwa wakati huu ambapo tunaona filamu ya Kiswahili imeshika kasi huku ikiwa inazidi kupunguza suala la usomaji kwa Watanzania. Kipindi hiki tunaona watayarishaji wengi wa filamu hasa vijana wakiwa wamepata uwanja mkubwa usio na vikwazo vya kutokuwawezesha kutamba hadithi zao pindi tu wanapokuwa na vifaa vya kiteknolojia vinavyowawezesha kuyanasibu mahangaiko yao ya kijamii wanayoyapitia kila uchwao. Changamoto kubwa kwa vijana hawa imekuwa ni kujivika majukumu mengi kama vile; uandishi wa miswada ya filamu pamoja na utayarishaji mzima wa filamu yote ikilenga kwenye uinuaaji wa kipato. Hilo si jambo baya kibiashara kwa ulimwengu wa sasa ambao watu wengi hutazama kiasi gani cha kipato utakachoingiza na si weledi ama ubora wa kazi (sanaa) unayoiunda, lakini kiujiu jambo hilo limekuwa ni lenye kutia mashaka hususani katika ukuaji wa lugha ya kiswahili, falsafa na utamaduni wa Mtanzania.

Licha ya filamu ya Kiswahili kuwa na faida kubwa sana katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili hasa kwa nchi zinazotuzunguka na hata katika umajumui, bado kuna jambo la muhimu la kutazama kuhusu lugha na utamaduni upi wa kitanzania unaotolewa na filamu hizi pamoja na eneo lingine kubwa la ukuaji wa lugha yenyewe (Kiswahili). Tumeona namna usomaji wa kazi za kifasihi ulivyopungua kwa kiasi kikubwa katika miaka ya 1990-hadi hivi sasa tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya 1960-1980. Hili halipo katika utamaduni wa Kiswahili pekee bali hata kwa sehemu kubwa ya bara la Afrika. Mathalani tukichukulia nchi ya Naijeria ambayo nayo hapo awali ilikuwa na utaratibu mzuri wa usomaji na uandishi wa kifasihi iliyojichanua vizuri kwa mifano ya *Onitsha Market of Literature*¹⁰ na *Kano Market of Literature*¹¹ ambayo ililikuza eneo la

¹⁰ *Onitsha Market Literature* inajumuisha hadithi fupi, michezo ya kuigizwa, pamoja na vitabu vya mafunzo ya kijamii vilivyokuwa vikitolewa mwanzoni mwa miaka ya 1960 na kuendelea kupitia waandishi wa ndani na kuuzwa katika soko la mji wa Onitsha uliopo katika Jiji la Anambra. Mji huu ulikuwa ni muhimu kibiashara kwa watu wa jamii ya Ki-Igbo wanaopatikana kusini mashariki mwa nchi ya Naijeria.

¹¹ *Kano Market Literature* wakati mwingine huitwa *Soyayya Books* (Vitabu vya hadithi za kimapenzi) au riwaya za kisasa za Ki-Hausa zilizokuwa zikipatikana katika mji wa Kano ulio kaskazini mwa nchi ya Naijeria.

fasihi nchini humo. Kwa sasa, makavazi hayo ya kiusomaji nchini Naijeria yako taabani. Hilo nalo limeikumba Tanzania ambayo zamani usomaji ulikuwa ni sehemu ya kujiburudisha kwa wasomi wa juu, wa kati, na hata wote walio kuwa wanauwezo wa kusoma. Kuingia kwa utandawazi, soko huria, uwepo wa mfumo mpya wa kiuongozi (Vyama vingi) na kuibuka kwa vituo vya runinga na filamu mwanzoni mwa miaka ya 1990 kumeonekana kuleta madhara katika maendeleo ya fasihi andishi na utamaduni wa usomaji.

Awali, kulikuwa na wachapishaji wengi waliokuwa radhi kujitumbukiza katika utoaji wa vitabu vya kifasihi lakini sasa kutokana na kudorora kwa usomaji tunaona wengi wamehama na kukimbilia katika uchapishaji wa vitabu vinavyotumika katika kufundishia katika ngazi za sekondari, vyuu vikuu, vitabu vya kisiasa, vitabu vya kutia moyo na tawasifu za viongozi na watu mashuhuri. Sanaa nyingine za kifasihi kama tamthiliya na riwaya zimebaki kuwa mashakani. Kwa hakika ufundishaji wa lugha katika mifumo rasmi ya kielimu ni jambo awali na lililo na umuhimu. Hivyo hivyo, ufundishaji wa lugha katika mifumo isiyo rasmi nalo ni jambo kubwa tena lenye manufaa mapana pia. Kupitia njia hii ya pili mwanafunzi wa lugha hupata wasaa wa kuitumia lugha katika mawasiliano kwa wazungumzaji wa lugha hiyo na kuweza kufanya mawazo yake yawafikie wazungumzaji wenzake wa lugha wanayoizungumza kwa pamoja. Mkondo huu wa pili wa ukuzaji lugha unahitaji umahiri wa njia nne za ufundi wa lugha ambao ni: kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

Katika njia hii ya pili, tunaona kuwa mtu anaweza kujifunza lugha vyema kwa kupitia mifumo ya kifasihi na kuyapata mawazo na falsafa mbalimbali ikiwa ana ufahamu wa kusoma. Kwa udondokaji huu wa usomaji tumeona “fasihi iliyopevuka” ikijidhihiri pekee huku bado ikiwa imeachwa pweke katika kufundishwa katika masomo ya fasihi ya lugha ya kiswahili. Katika mitalaa mingi ya lugha kuanzia ngazi za awali mpaka vyuoni hakuna uwepo wa somo hili hasa la uandishi wake (filamu) wa lugha ya kiswahili ili uweze kutoa mbinu kwa waandishi watakaoweza kufanya mawasiliano bora kwa watazamaji wao na papo hapo kutoa falsafa zitakazoboresha ukuaji bora wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Mtanzania.

Somo la uandishi wa sanaa ya filamu, vyuoni limeachwa katika Idara za Sanaa za Maonesho na Filamu ambako hufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Wasomi hao wanaojifunza kwa Kiingereza hujikuta katika mazingira ambayo huwapasa kuandika katika lugha ya Kiswahili wanapomaliza elimu zao kwani huko ndipo soko lao kubwa lilipo. Hivyo basi, tunajikuta tukiwapata

wasomi wengi waliotayarishwa vyema kiuandishi kwa lugha ya Kiingereza wanaokwenda kuandika filamu zao kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hakika hilo ni jambo la kushangaza na hatari kwa ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Jambo jingine, vijana wengi waliopo kiwandani kutayarisha filamu huandika filamu kwa uwezo haba wa kuweza kukuza lugha ya Kiswahili kutokana na mbinu finyu za lugha walizo nazo. Kwao uwepo wa vifaa vya kiteknolojia ni msingi tosha kwa kutamba hadithi zenye kukosa njia bora za fasihi na lugha katika kuyasema maudhui ya filamu zao pamoja na kueleza vyema utamaduni wa Mtanzania. Tukumbuke kueneza lugha kupitia filamu ni jambo la kwanza, lakini kukuza lugha kupitia filamu ni jambo jema zaidi.

Katika nchi nyingi, kwa njia za kiweledi, watayarishaji filamu huwafuata waandishi au wachapishaji mahiri wa kazi bora za kifasihi ili kuwaomba waweze kuwaruhusu kuzitumia kazi zao katika mfumo wa picha jongefu kwa njia ya filamu. Kuna faida kubwa kwa kuzihamisha kazi bora za fasihi andishi kwenda katika mfumo wa filamu. Uhamishaji huu huwa na manufaa ya kielimu, kiutamaduni, kisomi na hata kibiashara katika kuongeza uchumi. Kwa kuongezea, kuziweka kazi hizo za kifasihi katika mfumo wa filamu kutazidishia umaarufu kazi hizo za kibunilizi na kuwa kichocheo cha kunyanyua utamaduni wa usomaji pamoja na kuleta mvuto kwa jamii kuipenda taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine kutakuwa na faida kubwa kwa walimu wa masomo ya fasihi ya Kiswahili kuitumia teknolojia ya uwepo wa filamu katika kuongeza uwezo wao kiufundishaji na mbinu za kufundisha darasani kwa usaidizi wa filamu zitakazokuwa zimehifadhi kazi maarufu za kifasihi. Ukuaji wa kiteknolojia utawasaidia kufanya mawasilisho yao kwa njia za kieletroniki na kuongeza thamani katika kanuni za ufundishaji.

Tunafaa kutambua kuwa ni muhimu kuinua sanaa nyingine za kifasihi ili kuweza kukuza lugha ya Kiswahili na kuifanya isiwe lugha ya kununulia bidhaa sokoni ama kutumika kwa mawasiliano ya kawaida kama kama ilivyo hivi sasa bali kuifanya kuwa lugha yenye kutolea tajriba na falsafa zetu. Hivyo hivyo, pia hatuna jinsi zaidi ya kuongeza kisomo katika uandishi wa filamu ya Kiswahili katika kuongeza ujuzi wake katika kufanya mawasiliano bora, kutueleza vyema, kuikua na kuieneza lugha yetu adhimu ya Kiswahili na kuutambulisha utamaduni wa Mtanzania katika jamii nyingine za kilimwengu. Tumeona hivi kwa sababu jamii yeyote ya kilimwengu inayojitambua hutumia sanaa zote kwa mpigo katika kujiendeleza na kujiletea mafanikio. Jamii hizo hufahamu kuwa sanaa ni sehemu ya utamaduni na ni kiini cha mafanikio ya jamii yeyote. Mpaka hivi sasa licha ya uwepo wa sanaa ya filamu katika jamii zao bado haujaweza kuua sanaa nyingine na pia bado hazijaweza kudondosha utamaduni wa kujisomea kama sehemu ya kujipatia tulizo. Hii ni kinyume kabisa na ilivyo huku kwetu hususani kwa kipindi hiki cha usasa, teknolojia, soko huria, na utandawazi

kwa upana wake. Kipindi hiki utamaduni wa usomaji wa kazi za kifasihi umetupwa kando.

Hitimisho

Utamaduni wa Ki-Afrika katika makavazi pamoja na maktaba zake una hazina kubwa ya simulizi za kijadi ambazo zingeweza kuwa amali kubwa kwa filamu za Kiswahili za Ki-Tanzania. Bunilizi hizi ni hadithi mujarabu iwapo zingepewa nafasi katika uandishi na utayarishaji wa filamu za Kiswahili. Haitoshei hapo tu, kuna riwaya nyingi za Kiswahili ambazo nazo ingekuwa vyema zikihamishwa kutoka kwenye uasili wake yaani maandishi na kisha hadithi zake kutambwa kwa kutumia ufundi wa sanaa ya filamu ili maudhui na ujumbe unaozitoa uweze kuifikia jamii kubwa zaidi. Hii ni changamoto kwa watayarishaji wa filamu waache kutumia hadithi za filamu za kuigwa kutoka katika mazingira na jamii nyingine za kidunia. Waache kutumia motifu mfano za Ki-Naijeria na kwingineko katika kuumba kazi ya Kiswahili ambayo inatarajiwa kwenda kwa Mtanzania na wazungumzaji wengine wenye kuuishi utamaduni wa Kiswahili. Wanachopaswa kufahamu ni hivi: wana utamaduni wenye urithi mkubwa wa jamii mbalimbali zinazopatikana katika Tanzania na Afrika Mashariki kwa upana wake. Hadithi zipo zimesheni ndani ya utamaduni huo wa kipekee. Hawana namna ya kwenda mbali kutafuta hadithi za kutamba katika filamu wakati tayari utamaduni wao una hadithi tosha za kusimulia. Wajione kuwa wao ni watambaji wa kijadi waliobahatika kuishi katika maisha ya usasa. Wakumbuke kuwa hadhi yao imekuwa. Wametoka utambaji wa kijadi na kuwa waongozaji wa filamu zilizobeba hadithi wanazozitamba kila uchwao. Wana-jukumu kubwa kuulinda utamaduni wa Kiswahili na nchi ya Tanzania . Wao ni watu wenye wajibati kubwa ya kuhifadhi historia ya jamii pamoja na kuwa washauri wakubwa wa jamii. Wanalo deni kubwa la kuihuisha historia na idili njema za Kitanzania kwa kizazi na vizazi.

Watambaji manguli wa fasihi simulizi nao wasione kuwa wakati wao umeshamezwa na nguvu za kimawasiliano za jamii ya leo. Wasione kuwa wamepoteza wajibu wao wa kijamii. Wafahamu kwamba kwa sasa kuna uwanja mkubwa uliosheheni mifumo mingi ya kiwasiliano ya kisasa ambayo wanaweza kuitumia katika utambaji wa hadithi zao. Njia hizi za kisasa za kiteknolojia zilizoundwa kieletroniki huweza kupita moja kwa moja katika nyumba za watu na kutamba yale yaliyokusudiwa kupelekwa kwa jamii. Watambaji/Manju wana jukumu la kuzitumia njia hizo ili waweze kusikika. Kwa jinsi sanaa ya filamu inavyoonekana kuwa ni fasihi iliyostawi, ni njia mahiri ya kuijenga, kuisafisha na kitija kuitengeneza upya jamii ya leo.

Kama ilivyoada, fasihi hutumia lugha, taswira na wakati mwingine matendo kuyakinisha maudhui yake lakini filamu hutumia lugha, matendo na picha dhahiri zinazoonekana machoni mwa mtazamaji kudhihirisha maudhui yake yenye

nasaba ya kifasihi. Hivyo filamu hasa ya Kiswahili ikijengewa misingi bora inaweza ikatumika vyema kimasiliano kwani kitija athari yake ni kubwa na ya papo kwa hapo. Chambilecho, Mulokozi (1983, 2003) kwa ufupi, fasihi simulizi bado inapendwa, inatendwa, inahitajika na inatumiwa. Bado haijafa, na haitakufa siku za karibuni. Yumkini kamwe haitakufa kabisa, bali itabadilika tu na kuoanishwa na uandishi na teknolojia ya *media* ya umma.

Marejeleo

- Abiodun, O. (2011). Nollywood at the Borders of History: Yoruba Travelling Theatre and Video Film Development in Nigeria in *Journal of Pan African Studies*, Vol.4, No.5.
- Boggs, J., & Petrie, D. (2000). *The Art of Watching Films*, 5th edn. California: Mayfield Publishing Company.
- Brockett, O. (2003). *History of Theatre*. Boston: Allyn & Bacon.
- Cham, M. (2002). Film and History in Africa: A Critical Survey of Current Trends and Tendencies, Conference paper, University of Cape Town, South Africa.
- Diang'a, R. (2013). "Analysis of Style and Content in Selected Kenyan Films 1980 to 2009", PhD Thesis, Kenyatta University (Unpublished).
- Diawara, M. (1992). *African Cinema: Politics & Culture*, Indiana: Indiana University Press.
- Durotoye, A. A. (2003). Culture, Art and Film in an African Society: An Evaluation in *Nordic Journal of African Studies*, 12(1), 49-56.
- Hussein, E. (1983, 2003). "Makala za Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III". Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.
- Hussein, J. W. (2005). The Functions of African Oral Arts: The Arsi-Oromo Arts in Focus. *African Study Monographs*, 26(1), 15-58.
- Innocent, E. U. (2011). The Representation of African Traditional Religion and Culture in Nigeria Popular Films in *Journal of Politics and Religion*, No. 1(V).
- Kasiga, G. (2013). *U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania: Chanzo, Sababu na Athari kwa Wa-Tanzania* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kasiga, G. (2008). Tanzania Growing Film Industry and Job Opportunities for Youth, Conference Paper, University of Regina, Canada.
- Keyan, T., & Maureen, E. (1995). Perspectives on Orality in African Cinema. *Oral Tradition*, NO. 10(1): pg. 111-128
- Kileo, S. (2011). *Nafasi ya Maudhui ya Filamu za Kiswahili katika Kuakisi Masuala Muhimu ya Kijamii* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, Dar es Salaam.

- Kimani, N. (2006). Fasihi Simulizi na Nadharia ya Fasihi ya Kiafrika, Fasihi ya Kiswahili, Twaweza Communication.
- Mahenge, E. (2016). *Drama za Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Mlaga, W. K. (2017). Fasihi Elektroniki: Matokeo ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Makala iliyowasilishwa katika Kongamano la II la Chalufakita, SUMAIT- Zanzibar, Tar. 3 – 5, Agosti 2017.
- Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ua Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi ya Kiswahili Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers LTD.
- Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi Teknolojia Mpya, *Swahili Forum*, No. 14: uk.197-206.
- Nyoni, F. P. (1998). *Conformity and Change: Tanzania Rular Theatre and Social Political Changes*, (Unpublished PhD Thesis), University of Leeds.
- Perrier, R. G. (Ed.). (1992). *From Fiction to Film*. Minnesota: Archie Publication.
- Thackway, M. (2003). *Africa Shoots Back: Alternative Perspectives Sub-Saharan Francophone African Film*. Indiana: Indiana University Press.